

## **Kitabu cha Esta**

### **MAZINGIRA**

Kitabu cha Esta kinahusika na wakati wa taifa la Israeli unaojulikana kama wakati wa baada ya kifungo cha Babeli (au *post-exilic-period*). Habari zilizoandikwa katika kitabu hicho zilitokea Uajemi wakati wa utawala wa mfalme Ahasuero ambaye pia alijulikana kwa jina la Xerxes I. Alitawala kuanzia mwaka wa 486 mpaka wa 465 k.K. (Kwa habari zaidi kuhusu wakati huo taz. maelezo ya mazingira ya kitabu cha Ezra).

Uajemi ulikuwa nchi ya utawala mkuu wa Wayahudi zaidi ya miaka 50 kabla ya enzi ya Ahasuero, ambapo Koreshi alishinda na kuteka Babeli (539 k.K.). Ingawa Koreshi aliwaruhusu Wayahudi waliofungwa kurudi katika nchi yao, wengi wao waliamua kubaki Babeli (au Uajemi, nchi ile ilivyoitwa wakati huo). Wao walihakikishiwa usalama na uhuru fulani katika nchi ya kifungo chao, kwa hiyo hawakutaka kukabiliana na wasiwasi na ugumu wa maisha mapya huko Yerusalemu. Wao pamoja na watoto wao waliendelea kuongeza mafanikio ya namna mbalimbali, lakini hawakuonyesha nia ya kuimarisha upya dini yao iwe nguvu ya kiroho katika maisha yao ya kitaifa.

Lakini Mungu bado alikuwa akiendelea kuwalinda watu wake. Kitabu cha Esta hakitaji jina la Mungu wala shughuli za kidini ambazo kwa kweli zingalitakiwa kuwa jambo la kwanza katika maisha ya Wayahudi. Hata hivyo kinaonyesha jinsi Mungu alivyoendelea kutawala mambo yao, kama walimkubali au sivyo. Yeye asingeruhusu watu wake waangamizwe.

### **MUHTASARI**

1:1-2:23

Kuinuliwa kwa Esta kuwa malkia

3:1-7:10

Mikakati ya kuwaangamiza Wayahudi

8:1-10:3

Shangwe ya Wayahudi